

62-0313 Madhihirisho

Maswali ya Jaribio la Kanda la YF

Hadi : Jumatatu tarehe 31/07/2023

Jina: _____

1. Ndugu Branham alikuwa anamzungumzia nani wakati aliposema, "Maombi yangu, na maombi maaminifu ni, kwamba sote tutaufikia mwisho wa safari tukiwa na ushuhuda kama aliokuwa nao."?

- Dada Shepherd
- Georgie Carter
- Hattie Wright
- Dada Bell

2. Mungu Aliyaumba maumbile Kwa Kusudi gani?

- Shauku ya Kuyaumba
- Ili aweze kuishi mle yeye mwenyewe
- Ili mwanadamu aweze kuishi ndani yake
- ili Wanyama waweze kuishi ndani yake

3. "Na mara nyingi, wakati tunapochanganyikiwa, kama tungeangalia tu kote kutuzunguka, unaweza kumwona Mungu _____."

- Kila Mahali
- Ndani ya Watu
- Katika Biblia
- Kanisani

4. Na kila kitu kipo hapa kutumikia kusudi fulani, kama tu vile tulivyo hapa kutumikia kusudi fulani.

- Kweli
- Uongo

5. Ni mti wa aina gani ambao ndugu Branham alikuwa amesimama karibu yake alipokuwa anazungumza na yule Kafiri.

- Mpichi
- Mchungwa
- Mpera
- Mtofaa

6. Akina Nani, wamekuwa, kwa neema ya Mungu, wamehamishwa kutoka kwenye mti wa mauti hadi kwenye mti wa Uzima.?

- Wayahudi
- Wamataifa
- Wale Waliozaliwa kwa Roho wa Mungu
- Wale Wanaopaza sauti na kunena kwa lugha mpya

7. Neno "Dhihirisho" Linamaanisha nini?

- Kutamka siri
- Kusema maneno mazuri
- Kufanya hisia ijulikane
- Kuficha hisia

8. J-u-a ndilo ufufuo wa uhai wote wa_____

- Mimea
- Binadamu
- Mnyama
- Mdudu

9. M-w-a-n-a anaonekana kuwa, mara nyingi, mbali sana. Lakini Yeye anapoanza kumulika, "Jua la haki litawazukia likiwa na uponyaji katika _____ Zake." Ndipo kila uhai, haidhuru umezikwa wapi, kwa kilindi jinsi gani, umbali gani majini, ama katika mchang'a, penye mawe, utafufuka kwa utukufu wa Mungu."

- Mbawa
- Miale
- Mikono
- Njia

10. Mungu huufufua Uhai Wake unapotumikia_____.

- Wenyewe
- Kusudi Lake
- Maskini
- Yote ya hapo juu

11. Mungu ni Mungu wa vitu vya namna nyingi.

- Kweli
- Uongo

12. Yeye alishuka katika mfano wa mwanadamu, kuonyesha kile Yeye alichokuwa. Akafanyika Mtu wa_____, ajuaye_____.

- Huzuni/Sikitiko
- Uweza/Baraka
- Umaskini/huzuni
- Magonjwa/Uponyaji

13. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

- Yohana 5:24
- Yohana 14:12
- Marko 15:2
- Waebrania 4:12

14. Dhihirisho kuu kuliko yote lilikuwa ni lipi?

- Karama Kanisani
- Miujiza
- Uponyaji wa Miili yetu
- Yesu Kristo

15. Mara nyingi imesemwa, kwamba, "Mtu hufa kabla ya wakati wake, ama kitu fulani, kwamba labda ni dhambi fulani waliyotenda. Walifanya kosa fulani." ndivyo ilivyo kwa Mkristo.?

- Ndiyo
- Hapana

16. "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Na ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili wangu, hata hivyo katika_____ wangu nitamwona Mungu, Ambaye nitamwona mimi mwenyewe."

- Utukufu
- Mwili
- Roho yangu
- Mbingu

17. Ayubu angeweza kuangalia chini na kuona ufufuo wa kitu gani kati wa haya hapa?

- Mbegu
- Miti
- Jua
- Yote Yaliyo hapo juu

18. Ni nani aliyesema "Mwili wangu utakaa katika tumaini, kwa sababu Yeye hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu; wala hataiacha nafsi Yake katika kuzimu."

- Ayubu
- Sulemani
- Isaya
- Daudi

19. Mauti ndiyo mwisho wa safari.

- Kweli
- Uongo

20. Ni akina nani ambao Mungu atawapa shauku ya moyo wao?

- Watakaotembea kwa unyovu mbele zake
- Wanaostahili hilo zaidi
- Wanaoomba
- Wanaopitia majaribu